









**ELIMIKA KUHUSU UGONJWA WA
HOMA KALI YA MAPAFU
UNAOSABABISHWA NA VIRUSI
VYA CORONA**

Kwa maelezo zaidi
Piga Namba: 199 au *199#
Huduma hii ni bure kwa mitandao yote

 Eilimu ya Afya  @eilimu_ya_afya  @elimuyaafya  Afya TV Online



Imetolewa na:
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
Kupitia Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma
Tovuti: www.moh.go.tz



Utangulizi

Homa kali ya mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona ni ugonjwa unaoambukizwa kwa kuingiwa na majimaji yatokayo kwenye njia ya hewa wakati mtu mwenye ugonjwa huu anapokohoa au kupiga chafya. Njia nyingine ya maambukizi ni kwa kugusa majimaji yanayotoka puani (kamasii), kugusa vitambaa au nguo zilizotumiwa na mtu mwenye maambukizi ya ugonjwa huu, au maeneo mengine yaliyoguswa na mtu mwenye Virusi vya ugonjwa huu.

DALILI ZA HOMA YA CORONA



Homa



Kikohozi



Kubanwa mbavu na kupumua kwa shida



Vidonda kooni



Kuumwa kichwa



Mwili Kuchoka

Matibabu

Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja, hivyo kama yalivyo magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi, matibabu hufanyika kwa kuzingatia dalili zilizopo na ufuatiliaji wa karibu.

Jinsi ya kujikinga na homa ya Virusi vya Corona

- Kaa umbali wa angalau zaidi ya mita 1 kati yako na mtu mwingine
- Funika mdomo na pua wakati wa kukohoa au kupiga chafya kwa kutumia kitambaa safi au sehemu ya mbele ya kiwiko cha mkono
- Epuka kugusana na mgonjwa mwenye dalili za homa na kikohozi
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono, kukumbatiana au kubusiana
- Epuka kujigusa macho, pua au mdomo
- Subiri au epuka safari zisizo za lazima kwenda kwenye maeneo yaliyo athirika na inapolazimu kusafiri pata maelezo ya kitaalamu kabla ya kuondoka
- Epuka misongamano
- Safisha mikono yako mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kwa dawa ya kutakasa mikono
- Ukiona mojawapo ya dalili za ugonjwa huu, wahi kituo cha huduma za afya
- Vile vile toa tarifa kwenye kituo cha huduma za afya unapo mtu mwenye dalili za ugonjwa huu au piga simu namba: 199 au *199# huduma hii ni bure kwa mitandao yote





ELIMIKA KUHUSU UGONJWA WA HOMA KALI YA MAPAFU UNAOSABABISHWA NA VIRUSI VYA CORONA

Ugonjwa huu huenezwa kwa kuingiwa na majimaji yatokayo kwenye njia ya hewa wakati mtu mwenye ugonjwa huu anapokohoa au kupiga chafya. Njia nyingine ya maambukizi ni kwa kugusa majimaji yanayotoka puani (kamasi).



DALILI ZA HOMA YA VIRUSI VYA CORONA



Homa



Kikohozi



Kubanwa mbavu na kupumua kwa shida



Kuumwa kichwa



Vidonda kooni



Mwili Kuchoka

JINSI YA KUJIKINGA NA HOMA YA VIRUSI VYA CORONA



Safisha mikono yako mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au tumia vitakasa mikono



Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono



Funika mdomo na pua wakati wa kukohoa au kupiga chafya



Epuka kugusa macho, pua au mdomo



Kaa umbali wa angalau zaidi ya mita 1 kati yako na mtu mwingine



Epuka misongamano

Kwa maelezo zaidi piga simu 199 au *199# huduma hii ni bure kwa mitandao yote



Elimu ya Afya



@elimu_ya_afya



@elimuyaafya



Afya TV Online



Imetolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto.
Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma



Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

LISHE NA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA

Mtu mwenye lishe duni
huwa na kinga mwili dhaifu
hivyo apatapo maambukizi
ya virusi vya Corona mwili
huwa na uwezo mdogo wa
kupambana navyo na hivyo
kupata madhara makubwa,
kuchelewa kupona na kwa
baadhi ya watu kupoteza
maisha.



Zaidi kuhusu **CORONA** piga
199 au *199#
Huduma hii ni bure kwa mitandao yote



Jikinge, wakinge wengine,
CORONA INAZULIKA

@elimu ya afya



elimu ya afya online tv



@wizara_afyatz www.moh.go.tz



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

JKINGE NA CORONA



Safiri pale tu inapokulazimu kufanya hivyo

Zaidi kuhusu **CORONA** piga
199 au *199#
Huduma hii ni bure kwa mitandao yote



Jikinge, wakinge wengine,
CORONA INAZUILIKA

@elimu ya afya



elimu ya afya online tv



@wizara_afyatz www.moh.go.tz